# UQAB
Jarida la



*Toleo 14 - Jamad-al-thani 1439 AH / Machi 2018 Miladi*

**Ushuru**

**Hali ya Kisiasa Nchini Kenya: Mgogoro wa Demokrasia**

**Usivutiwe na Mapambo ya Dunia Hii ya Mapito**

**Wanawake Hawana Hadhi Chini ya Nidhamu ya Kijambazi ya Kidemokrasia**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi - Halaqa 10**

**SWALI/JAWABU: Matukio ya Kisiasa Ndani ya Kurdistan na Iran**



## Demokrasia Yajishambulia Yenyewe Nchini Kenya Kwa Kuzusha Chuki na Mifarakano ya Kikabila

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 04/1439 H | Jumamosi, 17 Jumadal Uula 1439 H | 03/02/2018 M

# Demokrasia Yajishambulia Yenyewe Nchini Kenya Kwa Kuzusha Chuki na Mifarakano ya Kikabila

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Kenya imeangaziwa katika midani za kimataifa baada ya kiongozi wa Muungano wa National Super Alliance (NASA) Raila Odinga kujiapisha kama rais kwenye sherehe iliohudhuriwa na maelfu ya wafuasi wake siku ya Jumanne 30 Januari 2018. Hatua hii inayotajwa kwenda kinyume na katiba ya nchi hasa ikizingatiwa kuwa Uhuru Kenyatta tayari aliapishwa mnamo mwezi Novemba mwaka jana kama rais kufuatia uchaguzi wa Oktoba mwaka jana uliosusiwa na Odinga. Huku tukio hili likiendelea kuzusha mjadala, **Harakati ya Kiislamu ya Hizb ut-Tahrir** ingependa kusema yafuatayo:-

Sherehe imetoa taswira ya taifa la Kenya jinsi linavyougua maradhi mabaya ya mifarakano ya kikabila na kimaeneo inayotiwa chachu na wanasiasa wake. Licha ya fikra duni za kizalendo na utaifa zinazopigiwa debe mara kwa mara, ni bayana kuwa fikra hizi ni duni na kamwe haziwezi kuleta umoja wa kudumu baina ya watu. Isitoshe, ukabila, utabaka na umaeneo ni mojawepo ya mbinu za wanasiasa wa Kidemokrasia wanazotumia katika kufikia au kubakia kwenye madaraka. Na ukweli huu haushuhudiwi tu hapa Kenya bali hata mataifa makubwa kama vile Marekani kama anavyoonekana Rais Trump hadharani akitoa matamshi ya kiubaguzi. Isitoshe, utawala wake umesheheni wanasiasa wenye sera za kibaguzi na chuki dhidi ya wahamiaji wa kigeni hasa watu wenye asili ya Afrika na Waislamu.

Ni wazi kuwa licha ya mamlaka iliojipa jamii ya Kisekula ya kujitungia katiba na kanuni ni wazi kuwa viongozi wake hawaziheshimu katiba hizo bali huzifuata na kuzikiuka kulingana na maslahi. Huku upande wa serikali ukiitaja hatua ya Raila kuwa ni kinyume na katiba, kwa upande wake, Raila na wafuasi wake nao wanadai kwamba hatua hiyo ilifuata katiba! Vioja havishii hapo; hatua ya serikali ya kuzima vyombo vya habari na kuwatolea vitisho wanahabari kwa kupeperusha hafla ya NASA inakiuka katiba huku vyombo hivyo vikitaja ni haki yao ya kikatiba kupeperusha matangazo. Ndio hivi ndivyo udhaifu wa kanuni za kibinadamu; wanaozitunga na kudai kuzilinda ndio hao hao huzikiuka na kuzivunja.

Twatoa tahadhari kwa Jamii ya Kenya kwa ujumla na hasa ya Kiislamu isitumbukie kwenye mtegano huu wa baina ya NASA na JUBILEE kwani kiasili ni sehemu tu miongoni mwa hila za wanasiasa wa kibepari jinsi wanavyoshindania nafasi ya kukimu na kushibisha matumbo yao huku wao kama walalahoi huambulia patupu! Ukweli ni kwamba mirengo yote hii huungana na kutengana kwa ajili ya maslahi. Tuliona hivi majuzi jinsi walivyoungana pamoja bungeni kujipa nafasi ya kujizolea kitita cha Shilingi 2.1 Bilioni kujinunulia magari ya kifahari huku gharama za maisha zikiendelea kupanda!

Twatamatisha kwa kukariri kuwa Uislamu pekee ndio ulio na uwezo wa kuzalisha siasa bora na wanasiasa wazuri wenye sera za kuleta ufanisi wa kisiasa, kiuchumi na kijamii kama ilivyoshuhudiwa kwa karne kumi na tatu wakati wa utawala wa Khilafah. Nasi tunaamini, na In Shaa Allah itarudi tena Khilafah hivi karibuni kuongoza tena dunia kwa siasa ya kweli itakayojaza ulimwengu mzima haki na uadilifu.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari**
**Hizb ut-Tahrir Kenya**

# Ushuru




## Utozaji 'Ushuru' ni nini?

Utozaji ushuru inamaana ya ukusanyaji pesa wa lazima au wa kinguvu wa mamlaka ya utozaji huo, aghalabu huwa ni serikali. Neno 'utozaji ushuru' hutumika katika aina zote za kodi za lazima, kuanzia katika mapato mpaka katika rasilimali na majumba. Utozaji ushuru hutofautiana na aina nyenginezo za malipo, kama ubadilishanaji masokoni, ambapo utozaji ushuru hauhitaji ridhaa na wala haukufungika moja kwa moja na huduma zozote zinazo peanwa. Serikali hulazimisha utozaji ushuru kupitia nguvu ya vitisho isiyo dhahiri au ya dhahiri. Utozaji ushuru kisheria ni tofauti na utozaji haramu au udanganyifu kwa sababu taasisi inayotoza ni serikali na wala si watu binafsi.

Nidhamu za ushuru zimetofautiana pakubwa baina ya tawala na zama. Katika nidhamu nyingi za kisasa, utozaji ushuru hufanyika juu ya milki halisi, kama rasilimali, na matukio maalumu, kama muamala wa mauzo. Uundaji wa sera za ushuru ni mojawapo ya kadhia nyeti na zenye sintofahamu nyingi katika siasa za kisasa.

## Madhumuni na Uhalalishaji wa Utozaji Ushuru

Lengo msingi la utozaji ushuru ni kufadhili matumizi ya serikali. Kuna visingizio na ufafanuzi kadhaa wa kadhaa unaotumiwa kuhalalisha ushuru kwa muda wote wa historia. Ushuru wa kale ulitumika kufadhili matabaka ya watawala, majeshi na kujenga ulinzi. Aghalabu, mamlaka ya ushuru ilichipuza kutokana na haki ya kiroho. Baadaye, visingizio vya uhalalishaji ushuru vikapeanwa kwa vigezo vya umuhimu wake kiuchumi au kijamii. Utozaji ushuru ni nidhamu ambayo serikali huitumia kukusanya pesa kufadhili matumizi ya serikali. Serikali hutumia mapato ya ushuru kulipa mishahara ya jeshi na polisi, kujenga mabwawa na barabara, kuendesha shule na hospitali, kutoa chakula kwa masikini na matibabu kwa wakongwe, na mamia ya malengo mengine. Bila ya ushuru kufadhili amali zake, serikali hazingeweza kuwepo. Wanaotetea kuwepo kwa viwango vya ushuru wa kuendelea kwa wenye mapato ya juu wanajadili kuwa ushuru hushajiisha kuwepo kwa jamii iliyo na usawa zaidi. Kiwango cha juu cha ushuru kwa bidhaa na huduma maalumu, kama tumbaku au pombe imedaiwa kupunguza matumizi yake.

Katika muda wote wa historia, watu wamejadili kiwango na aina za ushuru ambazo serikali inatakiwa kutoza, pamoja na namna inavyo takikana kugawanya mzigo wa ushuru huo kwa jamii nzima. Ushuru usiokuwa wa kawaida umesababisha maandamano ya raia, ghasia, na hata mapinduzi. Athari ya utozaji ushuru kamwe sio tu ugurishaji wa mali. Nadharia za kiuchumi kuhusu utozaji ushuru zimelikabili swala la vipi kupunguza hasara ya kiuchumi kupitia utozaji ushuru na pia kujadili juu ya vipi taifa laweza kutekeleza upya ugavi wa mali kwa njia thabiti zaidi.

Serikali zimetoza ushuru aina nyingi. Katika nchi nyingi zanazo endelea, watu hulipa ushuru wa mapato pindi wanapopata pesa, ushuru wa matumizi pindi wanapozitumia, ushuru wa rasilimali pindi wanapomiliki nyumba au ardhi, na katika baadhi ya hali ushuru wa milki pindi wanapokufa. Wale wanaolipa ushuru kwa msingi wa mpangilio huu kiujumla hupoteza asilimia 50%-60% ya mishahara yao kwa utozaji ushuru. Nchini Amerika, majimbo, serikali kuu, na serikali za mitaa zote hukusanya ushuru. Ushuru katika mapato ya watu hucheza dori

*Endelea Uk..4*

muhimu katika nidhamu ya mapato kwa nchi zote zilizo endelea. Nchini Amerika, ushuru wa mapato ya mtu binafsi ndio kitovu kikuu cha mapato ya serikali. Mnamo 2010 ulifikia kiwango cha asilimia 47% ya mapato ya majimbo yote.

Katika makala kwa anwani Uislamu na Utozaji ushuru ya Adnan Khan kwa tovuti ya Khilafah.com na yaliyo chapishwa mnamo 4th July 2009, alisema kuwa kiwango cha utozaji ushuru katika taifa lolote huathiri tabia za watu, ikiwemo machaguo yao katika kufanya kazi, kuweka akiba, na kuwekeza. Utozaji ushuru katika Magharibi umesababisha idadi ya matatizo katika ugavi wa mali ambapo mzigo huwaangukia pakubwa masikini huku matajiri wakitumia fursa ya mwanya na hifadhi za ushuru. Kiwango cha matumizi katika uchumi wowote huathiriwa na kiwango cha utozaji ushuru. Mzigo mkubwa wa ushuru waweza kuwa na athari mbaya kwa uchumi wote kwa jumla hususan katika Magharibi ambapo matumizi hucheza dori muhimu.

Maamuzi ya uwekezaji ya makampuni pia huathiriwa na utozaji ushuru kwa kuwa hupunguza mapato yake na hivyo kupunguza manufaa ya uwekezaji. Wanauchumi wengi wanaamini kuwa ushuru wa biashara hupunguza kiwango hisika cha uwekezaji kwa biashara. Ushuru pia huathiri aina za uwekezaji ambazo biashara hufanya. Hii ni kwa sababu serikali hutoza ushuri mapato ya baadhi ya aina za uwekezaji kwa kiwango cha juu kuliko nyengine. Tofauti hizi husababisha biashara kufanya maamuzi ya uwekezaji kwa msingi wa natija za ushuru, kuliko kuwa zinahalisi kwa mtazamo wa kibiashara. Kwa kuyaharibu maamuzi ya uwekezaji, nidhamu ya ushuru hupelekea kuwepo kwa mpangilio wa uwekezaji usio thabiti. Kimsingi, tatizo au mjadala unabakia kuwa je, utozaji ushuru unapaswa kuwa juu ya mapato au mali?

**Ushuru nchini Kenya – Mamlaka ya Utozaji Ushuru nchini Kenya (KRA)**

Mamlaka ya Utozaji Ushuru nchini Kenya iliasisiwa mnamo 1995 kupitia kanuni ya bunge, chini ya kifungu nambari 469 cha sheria za Kenya. Mamlaka hii inajukumu la kutathmini, kukusanya na kuhasibu ushuru. Hukusanya ushuru na kusimamia kanuni za mapato kwa madhumuni ya kufanikisha biashara. Mamlaka hii hukusanya aina nne za ushuru: ushuru wa forodha na utengezaji bidhaa za humu nchini, ushuru wa mapato, ushuru wa ununuzi bidhaa (VAT) na leseni za magari na madereva.  Zaidi ya hayo, chini ya nidhamu ya serikali za ugatuzi, kaunti zaweza kutoza ushuru fulani ndani ya mipaka yake.

Ushuru wa mapato ni wa zamani kama ulivyo ushuru wa forodha nchini Kenya. Ushuru zote hizi zilianzishwa nchini na serikali ya kikoloni na zimeendelea kuwepo tangu wakati huo. Kinyume na ushuru wa ununuzi bidhaa (VAT) na ushuru wa forodha na utengezaji bidhaa za humu nchini, ushuru wa mapato ni ushuru unaotozwa moja kwa moja juu ya watu na makampuni. Ushuru zote nyengine ni za njia isiyo moja kwa moja ambapo hazina uhusiano wa moja kwa moja na matumizi yako ya bidhaa na huduma zinazo tozwa ushuru pasi na kuzingatia kiwango chako cha mapato.

Ukusanyaji ushuru licha ya hayo haukosi sintofahamu juu ya kufikia kwake malengo yake au kukusanywa kwa njia thabiti. Benki ya Dunia katika toleo lake la 16 la Upashaji Upya wa Habari za Kiuchumi za Kenya ilisema kuwa ukuaji wa mapato ya ushuru ya Kenya ni wa kiwango cha chini ndani ya muongo mmoja. Taasisi hii ya utoaji mikopo ya kiulimwengu imegundua kuwa ingawa biashara imeongezeka katika bidhaa na huduma, ni chache kati ya amali hizi za kiuchumi ambazo hutozwa ushuru.  Hii imepelekea serikali kuwa na uhaba mkubwa wa mapato na hivyo kuitumbukiza katika madeni zaidi. Tarakimu kutoka kwa Hazina ya Kitaifa zaonyesha kuwa mwaka wa 2016/17, kiwango jumla cha ukusanyaji mapato, ikiwemo matumizi kutokana na misaada, kilikuwa shilingi 1.4 trilioni. “Mapato haya yalipungua kwa shilingi 54.8 bilioni chini ya shabaha iliyo lengwa ya shilingi 1.45 trilioni kutokana na upungufu katika ukusanyaji wa mapato ya kawaida kufuatia kupungua kwa ukusanyaji ushuru wa utengezaji bidhaa za humu nchini na ushuru wa mapato ya makampuni, na kupungua kwa ukusanyaji jumla wa mapato ya wizara (kwa shilingi 49.2 bilioni),” Hazina ilisema haya katika waraka wake wa kutathmini na kuangazia bajeti.

Waziri wa Hazina ya Kitaifa Henry Rotich alikuwa pia akichechemea kutoka changamoto moja ya kifedha hadi nyengine kwani mkopo ambao serikali uliuchukua miaka miwili iliyopita katika hali ngumu zaidi, kuwadia wakati wake wa malipo, huku kukiwa na uhaba wa pesa za kuulipa. Waziri Rotich ambaye hivi majuzi alifichua kwamba nchi itatoa zabuni nyengine ya Eurobond kulipa mkopo wa dolari 750 milioni (shilingi 77 bilioni) ambao ulitarajiwa kufikia wakati wake wa malipo mnamo Oktoba,alipata wakati mgumu kuwahakikishia Wakenya kwamba nchi haina matatizo ya kifedha. Huku muda wa malipo ya mkopo huo ukiwadia, Mamlaka ya Ushuru ya Kenya (KRA) ilikuwa na upungufu wa shilingi 40 bilioni katika shabaha yake ya mapato kutokana na kutolewa kwa ruzuku kubwa ya sukari, ngano, mahindi na maziwa iliyopelekea kuanguka kwa ushuru wa forodha. Upungufu kati ya bajeti na kile kilicho kusanywa na KRA umeendelea kukuwa kwa viwango vikubwa inayoifanya serikali kuwa vigumu kuendesha shughuli zake pasi na deni jipya. Mtoza ushuru pia atatafuta njia mpya za kutathmini ushuru na kuboresha upekuzi wa shehena huku wakati huo huo akipekua maelezo ya ziada yatakayo unganishwa na akaunti za benki, mfumo wa fedha wa kidijitali na Benki Kuu.

Kizungumkuti chengine katika sera ya utozaji ushuru chini ya urasilimali ni kufeli kwa serikali kudhihirisha

***Endelea Uk..5***



**Email: info@uqab.or.ke**

jinsi inavyotumia mapato yanayo kusanywa. Katika kongamano la tatu la ushuru la kila mwaka la Mamlaka ya Ushuru ya Kenya (KRA) lililofanyika mnamo Disemba 2017 katika Chuo Kikuu cha Nairobi, Bwana Nikhil Hira, mmoja wa wataalamu aliye pia mshauri wa maswala ya ushuru katika kampuni ya Deloitte alijadili kuwa maadamu serikali haifanyi uhasibu wa wazi wa jinsi inavyotumia mapato yaliyo kusanywa, watu kamwe hawatahisi uwajibu wa kulipa ushuru.

Katika toleo la 'Jibu la Swali' la Hizb ut Tahrir kwa anwani "Stakabadhi za Panama zilizo fichuliwa na madhumuni yake", ilielezwa kuwa sera ya utandawazi iliyofuatilizia na Amerika wakati wa muhula wa Raisi Clinton ilipelekea wamiliki wengi wa mtaji wa Kiamerika kuweka mali zao nje ya mipaka ya nchi hiyo. Amerika inataka kuvunja vikwazo baina ya nchi na kuzikoloni kiuchumi. Imefaulu katika kudhibiti fedha kupitia utandawazi, lakini kwa upande mwengine, warasilimali wa Kiamerika wamepata njia nyengine ya kukwepa utozaji ushuru wa Amerika. Ili kukamilisha nidhamu ya utandawazi na kufanikisha utembeaji wa mtaji, kuanzishwa kwa aina mpya ya makampuni baina ya nchi kwa jina kampuni za "ng'ambo" kuliibuka ambapo ziliandikishwa katika nchi mmoja lakini utendakazi wake unafanyika katika nchi nyengine. Zinaweka pesa zake katika nchi ya tatu lakini zinaweza kuendesha shughuli zake katika nchi ya nne. Hivi ndivyo kampuni hizi za "ng'ambo" zinavyotumia majina ya wawakilishi wake, kama vile Mossack Fonseca au watu wengine kinyume na majina ya wamiliki wake halisi.
Ili kukweka kulipa ushuru, Matajiri wa Kenya wanajifunza kutoka kwa wenzao ulimwenguni katika kudumu kutafuta mipango fiche ya kuhifadhi pesa zao na kuziweka mbali kutokana na mtoza ushuru kwa gharama zozote ziwezekanazo. Kama ilivyo elezwa katika gazeti la Standard la mnamo Novemba 12, 2017, washauri wa kibinafsi wa ushuru hulipwa dolari za juu kubuni mbinu za kuanzisha uwekezaji kote ulimwenguni kupitia miundo ya umilikaji inayolenga kuzihadaa taasisi za utozaji ushuru. Sababu nyingi zimetolewa juu ya kuwepo kwa mipango hiyo mirefu na mipana ikiwemo uthabiti katika ulipaji ushuru na usiri kwa familia au washindani wa kibiashara. Lakini upendeleaji maeneo maalumu kibiashara kama Mauritius na Jersey umeangaziwa kwa umakinifu, ukitoa maelezo kwa mdahalo wa kiulimwengu juu ya dori ya maeneo haya katika kushajiisha ukwepaji ushuru na usiri. "Ni katika maslahi ya kila mmoja kulipa kiwango cha chini kabisa kiwezekanacho cha ushuru maadamu si haramu" alisema Muema, aliyekuwa mshirika katika kampuni ya ushauri wa kiulimwengu ya KPMG nchini Kenya.

**Je, Ushuru Unaruhusiwa Katika Uislamu?**

Kama ilivyo ndani ya kitabu cha Amwaal, ushuru (Maks) huchukuliwa licha ya kuwa kuna Hadith nyingi zinazo kataza ushuru (Maks) na zimetoa ukali dhidi ya mkusanyaji wake, mithili ya ile iliyo simuliwa na Uqba b. Amir kwamba amemsikia Mtume wa Allah (saw) akisema: "**Hataingia peponi mtozaji ushuru.**" Ushuru huu ni ule unaochukuliwa kutoka kwa wafanyi biashara wanapovuka mipaka ya serikali. Imesimuliwa pia na Kareez b. Sulaiman, aliyesema: "Umar b. Abdul Aziz alimuandikia barua Abdullah b. Awf al-Qari kuwa asafiri mpaka afike katika jumba lijulikanalo kama jumba la ushuru katika eneo la Rafah na kulibomoa, kisha alibebe mpaka baharini na kulitawanya tawanya. Alimuandikia barua Ady b. Arta'a kuondoa fidia, chakula na ushuru kutoka kwa watu kwa kuwa huo sio ushuru bali ni upunjaji (wa mali za watu) ambao Allah (swt) amesema:

وَلاَ تَبْخَسُوا النَّاسَ أَشْيَاءَهُمْ وَلاَ تَعْثَوْا فِي الأَرْضِ مُفْسِدِينَ (هود: 85)

Msiwakhini watu vitu vyao; wala msieneze uovu katika nchi mkafanya uharibifu [Hud: 85]

Hadith na ripoti zote hizi zinakataza ushuru (Maks), na zinakemea vikali dhidi ya mkusanyaji wake ishara ya uharamu wa ukusanyaji wake. Lakini, kuna ripoti nyengine zinazo ashiria kuwa 'Umar ibn Al-Khattab na Makhalifa baada yake, Uthman, Ali na 'Umar bin Abdul Aziz, walikuwa wakichukua Ushr kutoka kwa bidhaa zinazovuka mipaka ya serikali. Walikuwa wakichukua robo ya Ushr (asilimia 2.5%) kutoka kwa wafanyi biashara Waislamu, nusu ya Ushr (asilimia 5%) kutoka kwa wafanyi biashara raia wasiokuwa Waislamu (Dhimmi) na Ushr kamili kutoka kwa wafanyi biashara tulio katika vita nao (Harbi). Ripoti kutoka kwa Ziyad bin Hudayr yasema: "Umar ibn Al-Khattab aliniteua kusimamia Ushr na kuniamuru kuchukua robo ya Ushr kutoka kwa wafanyi biashara Waislamu." Na katika ripoti nyengine asema: "Umar ibn Al-Khattab aliniamuru kuchukua Ushr kamili kutoka kwa manaswara wa Bani Taghlib na nusu ya Ushr kutoka kwa manaswara wa Ahl ul-Kitab."

Ripoti hizi ziko wazi kuwa 'Umar na Makhalifa baada yake, walikuwa wakichukua robo ya Ushr kutoka kwa wafanyi biashara Waislamu wanaovuka mipaka, nusu ya Ushr kutoka kwa wafanyi biashara raia wasiokuwa Waislamu (Dhimmi) na Ushr kamili kutoka kwa wafanyi biashara tulio katika vita nao (Harbi). Hili lilishuhudiwa na Maswahaba na kuliridhia, ikithibitisha Ijma'a yao juu ya kukubaliwa kuchukua. Vile vile 'Umar bin Abdul Aziz, aliye muamuru Ady bin Arta'a kuacha kuchukua ushuru kutoka kwa watu na Abdullah bin Awf al-Qari kulivunja jumba la ushuru eneo la Rafah, alimuamuru Wali wa Misri, Zareeq bin Hayyan al-Damashqi kuchukua robo ya Ushr kutoka kwa Waislamu na nusu ya Ushr kutoka kwa Dhimmi." Hadith na ripoti hizi zaonekana kugongana na hadith zilizotangulia zinazo kataza ushuru (Maks) kwa ukali na kukemea dhidi ya mkusanyaji wake, na pia zile zinazosema kuwa 'Umar na Ziyad hawakuwatoza ushuru Waislamu wala Dhimmi.

Uchunguzi wa makini wa Hadith na ripoti hizi juu ya kadhia hii waonyesha kuwa kamwe hakuna

Endelea Uk..6

mgongano baina yazo. Ushuru (Maks) iliyokatazwa kwa ukali dhidi ya mkusanyaji wake inakusudiwa pesa zinazo chukuliwa pasi na haki (kiharamu) kutoka kwa Waislamu kama kuchukua Ushr kamili kutoka kwao au kuchukua zaidi ya robo ya Ushr kutoka kwa wafanyi biashara wao wanaovuka mipaka. Ushuru si wajib juu ya Waislamu, wala hawawajibiki kutozwa chochote juu ya bidhaa zao isipokuwa Zaka, ambayo kiwango chake ni robo ya Ushr (asilimia 2.5%). Huu sio ushuru wa forodha (Maks) wala mwengine. Huu ndio ufafanuzi wa Hadith za ibn ‘Umar na Ziyad bin Hudayr kusema kuwa ‘Umar hakuchukua ushuru; badala yake alicho chukua ni Zaka kutoka kwao na kiwango chake ni robo ya Ushr (asilimia 2.5%) na wala Ushr kamili.

Ama kuhusu raia wasiokuwa Waislamu (Dhimmi), Ushr haikuchukuliwa kutoka kwao, kiwango kilicho chukuliwa ni nusu ya Ushr pekee. Nusu hii ya Ushr iliyo chukuliwa kutoka kwao ilikuwa ni sharti la mkataba wa amani (Sulh) uliofungwa baina yao na ‘Umar bin Al-Khattab wakati Iraq, Ash-Sham na Misri zilipo funguliwa. Hivyo basi, ushuru (Maks) iliyo haramishwa na mkusanyaji wake kukemewa vikali ni ule unaochukuliwa kiharamu kutoka kwa Waislamu na Dhimmi au Harbi, iwe ni kiwango zaidi ya kinacho takikana au kiwango kikubwa zaidi ya kinacho chukuliwa kutoka kwa wafanyi biashara Waislamu wanapo tembelea ardhi zao. Vile vile, Malik bin Anas alikuwa akipenda kusema: “Waliekewa mkataba wa kuishi ndani ya ardhi zao, kwa hivyo kila wanapo vuka kwa ajili ya biashara hawana budi kutozwa ushuru.” Kwa hivyo imekuwa wazi kwamba hakuna mgongano na ushuru (Maks) uliokatazwa ni ukusanyaji wa mali kiharamu. Ushuru unaochukuliwa kutoka kwa wafanyi biashara Dhimmi na Harbi ni ngawira kwa Waislamu. Huwekwa katika diwani ya ngawira na Kharaj na hutumiwa kama matumizi ya Jizya na Kharaj.

**Utozaji Ushuru Katika Uislamu**

Ushuru ni mali zilizo wajibishwa juu ya Waislamu na Allah (swt) ambazo ni muhimu katika kukidhi mahitaji na maslahi yaliyo wajibishwa juu yao katika hali ambapo kuna uhaba wa fedha katika Bait ul-Mal ya Waislamu kusimamia mahitaji na maslahi haya. Uislamu una mtazamo tofauti juu ya uchumi na ushuru kwa kuwa msingi wa Uislamu ni tofauti na ule wa urasilimali. Kimsingi utozaji ushuru katika Uislamu na chini ya Khilafah hutilia mkazo utozaji ushuru katika mali badala ya mapato. Nidhamu ya utozaji ushuru ya Kiislamu haitozi ushuru mapato, bali hutoza ushuru mali. Hii ina maana kuwa mtu mwenye kiwango cha wastani ataachwa akiwa na mapato zaidi ya kutumia na atawajibika juu ya ushuru katika kiwango cha ziada kitakacho bakia mwishoni mwa mwaka. Hili litakuwa na athari kubwa juu ya uchumi.

Kiasili, machimbuko ya kudumu ya mapato ya Bait ul-Mal ambayo Allah (swt) amepitisha kuwa wajib juu ya Waislamu, ni kutoka katika Fai’, Jizya, Kharaj, Ushr na pesa kutoka katika mapato ya mali za umma zilizo hifadhiwa na dola, zapaswa kuwa za kutosha kuhakikisha uwajibikaji wa matumizi ya Bait ul-Mal juu yake. Lakini, Allah (swt) amejaalia matumizi juu ya mahitaji na maslahi haya ambayo Bait ul-Mal imewajibishwa kuyakidhi iwe kuna mali ya kutosha ndani yake au la, kuwa jukumu juu ya Waislamu endapo kutakosekana fedha ndani ya Bait ul-Mal kukidhi mahitaji haya.

Mzigo mkubwa utakaokuwa juu ya dola ya Khilafah leo huenda ukayafanya machimbuko ya kudumu ya mapato ya Bait al-Mal kutototosheleza kusimamia matumizi yote kwa mahitaji na maslahi yaliyo wajibishwa kwake. Ikiwa machimbuko haya ya mapato hayatatosheleza, na hakuna fedha ndani ya Bait al-Mal na hakuna Waislamu wanaojitolea kuchangia kwa khiari ili kusimamia mahitaji na maslahi haya, jukumu hili litagura kutoka kwa Bait al-Mal na kuwaangukia Waislamu. Hii ni kwa sababu Allah (swt) amewawajibisha kukidhi mahitaji na maslahi haya, na kufeli kwao kukidhi mahitaji na mambo haya itapelekea kudhurika kwa Waislamu, ambapo Allah Ta’ala ameiwajibisha dola na Umma kuondoa madhara yoyote kutoka kwa Waislamu. Mtume (saw) amesema: “**Hakuna kudhuru wala kudhuriwa**.” Hivyo basi Allah ameiwajibisha dola kukusanya pesa kutoka kwa Waislamu kusimamia matumizi juu ya mahitaji na maslahi haya.

Ikiwa hali hii itaibuka, basi dola ni lazima itoze ushuru juu ya Waislamu kiasi ya kuwa matumizi ya lazima juu ya mahitaji na maslahi haya yashibishe pasi na kuzidisha ukusanyaji. Dola ni sharti ikusanye ushuru huu kutokana na ziada inayobakia katika mahitaji ya watu msingi na ya ziada kwa mujibu wa viwango vya kawaida vya kimaisha. Yafuatayo ni maslahi yanaofadhiliwa na Bait al-Mal, au kupitia utozaji ushuru kwa Waislamu endapo hakutakuwepo na fedha ndani ya Bait al-Mal.

1. Matumizi juu ya Jihad na yanayo lazimu juu yake. Haya yanajumuisha uundaji wa jeshi imara na kulipa kiwango cha mafunzo ya hali ya juu, kulitayarisha kwa zana imara kiasi ya kuwa idadi na ubora wake itawavunja moyo, kuwashinda na kuwahofisha maadui, kuzikomboa ardhi zetu na kumaliza ushawishi wa makafiri katika ardhi za Waislamu na kuliwezesha pia kulingania Uislamu ulimwengu mzima. Ikiwa hakuna fedha, basi jukumu hili la kutumia kwa ajili yake, maadamu Jihad ni faradhi na imesimama, litagura kutoka kwa Bait al-Mal kwenda kwa Waislamu, kwani Jihad ni wajib juu yao kwa mali na nafsi. Allah (swt) asema:

انفِرُوا خِفَافًا وَثِقَالاً وَجَاهِدُوا بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ

Nendeni mtoke, mkiwa wepesi na wazito, na piganeni Jihadi kwa mali yenu na nafsi zenu katika Njia ya Mwenyezi Mungu. Haya ni kheri kwenu mkiwa mnajua. [At-Tauba: 41]

Anas amesimulia kwamba Mtume wa Allah (saw) amesema: “**Piganeni**

*Endelea Uk..7*

**na washirikina kwa mali zenu, mikono yenu na ndimi zenu**." Kuongezea, kuna makumi ya Aya na Hadith zinazo wajibisha Jihad kwa mali na nafsi juu ya Waislamu. Ikiwa michango ya Waislamu haitatosha kusimamia juu ya Jihad iliyo simama, basi dola itatoza ushuru juu ya Waislamu kujaliza kiwango kinacho hitajika na wala si zaidi ya hapo.

2. Kutoa kwa ajili ya masikini, mafukara na wasafiri. Hili ni wajib kuweko na fedha au kusiweko na fedha ndani ya Bait al-Mal. Hii ni kwa sababu kutoa kwa ajili ya masikini, mafukara na wasafiri imewajibishwa na Allah juu ya Waislamu kwa njia ya Zaka na Sadaka. Mtume wa Allah (saw) anasimulia kutoka kwa Mola wake: "**Yeyote anaye kwenda kulala akiwa ameshiba ilhali anajua jirani yake ubavuni mwake ana njaa bado hajaniamini mimi**."

3. Gharama kama mishahara ya wanajeshi, watumishi wa Umma, makadhi, walimu na mfano wao wanaotoa huduma kwa manufaa ya Umma. Wanastahili, kama badali ya utoaji wao huduma hizi, mishahara kutoka kwa Bait al-Mal, na haki ya kutoa kwa ajili yao ni wajib kuweko na fedha au kusiweko na fedha ndani ya Bait al-Mal. Hii ni kwa sababu Allah (swt) amepitisha utawala (Sultan) uwe kwa Umma na kuuwajibisha kumteua Khalifah watakayempa ahadi ya utiifu (Bay'ah) kumsikiza na kumtii kwa mujibu wa Kitabu cha Allah na Sunnah za Mtume wake (saw). Khalifah huyu hutekeleza utawala wake kwa niaba yao na kusimamia mambo yao kwa mujibu wa Kitabu na Sunnah. Usimamizi wa mambo yao waweza tu kutimia kwa kupitia kubuni taasisi za dola, zikiwemo taasisi za serikali kama makadhi, wanajeshi, walimu na watumishi wa Umma. Kuteua watu kama hawa ndani ya dola yahitaji malipo ya ridhaa na mishahara. Kwa kuwa Allah amewawajibisha Waislamu kuwateua watu kama hawa, basi Yeye (swt) pia amewawajibisha kuwalipa ridhaa na mishahara yao kwa njia isiyokuwa na budi. Mtume wa Allah (swt) aliyeteua ma-Wali, waajiriwa, makatibu na kuwatengea malipo ('Atiyyat) yao. Vile vile Makhalifa baada yake waliteua ma-Wali, maafisa, makadhi, makatibu na wanajeshi, na kuwatengea malipo yao kutoka kwa Bait al-Mal au kwa kutoza ushuru unaohitajika juu ya Waislamu wakati ambapo Bait al-Mal ilikuwa na upungufu wa fedha kutekeleza lengo hili.

4. Gharama zinazo hitaji kulipwa kwa muundo wa huduma na usimamizi wa Umma. Hizi hutolewa kwa ajili ya huduma za jamii ambazo kuwepo kwake kunakadiriwa kuwa dharura kiasi cha kuwa kukosekana kwake hupelekea madhara kwa Umma. Hudumu hizi zinajumuisha barabara za Umma, shule, vyuo vikuu, hospitali, misikiti, usambazaji maji na huduma nyenginezo mithili ya hizi.

5. Matumizi juu ya matukio ya dharura kama ukame, mitetemeko ya ardhi, mafuriko na mashambulizi ya adui. Haki ya kutoa kwa ajili ya mambo haya haitegemei kuweko kwa fedha ndani ya Bait al-Mal. Utoaji huo ni wajib pasi na kujali kuweko na fedha au kusiweko na fedha ndani ya Bait al-Mal. Ikiwa kuna hofu ya kutokea madhara endapo yatacheleweshwa, basi dola itakopa kiwango kinacho hitajika kutumika juu ya dharura hizi na kisha kulipa ilicho kopa kutokana na kile itakacho kusanya kutoka kwa Waislamu. Dalili ya kuwajibisha hili juu ya Waislamu ni Hadith: "**Mkataba wa Allah huondolewa kutokana na watu wa eneo lolote ambalo muna watu wenye njaa.**"


Ushuru huchukuliwa kutoka kwa mali ya Waislamu iliyozidi mahitaji msingi na ya ziada kwa mujibu wa viwango vya kawaida vya kimaisha. Hakuna kinacho chukuliwa kwa wale wasiokuwa na ziada katika mali yao. Hii ni kutokana na maneno ya Mtume (saw): "Sadaqa bora ni ile inayotolewa kutokana na utajiri." Utajiri hapa una maana ya kile ambacho mtu anakimudu baada ya kushibisha mahitaji yake. Dola hairuhusiwi kutoza ushuru usiokuwa wa moja kwa moja, wala kufanya hivyo kwa njia ya ada za mahakama, ada za rufaa zinazo wasilishwa kwa dola, uuzaji au uandikishaji wa ardhi, majengo au vipimo au aina nyengine za ushuru tofauti na zile zilizotajwa tayari. Hii ni kwa sababu kukusanya ushuru huo ni miongoni mwa dhulma zilizo haramishwa na ambazo Mtume (saw) amezungumzia kuzihusu akisema: "Haingii Peponi mkusanyaji ushuru."

**Mukhtasari**

Ni wazi kuwa sera za utozaji ushuru zinazo tekelezwa ndani ya nidhamu ya kirasilimali zimefeli kufikia malengo yao kwa kuwa pesa zinazo kusanywa kamwe hazitumiki vizuri na vipimo vinavyo tumika si vya usawa. Zaidi ya hayo, serikali haifanyi uhasibu wa wazi wa namna inavyo tumia mapato yanayo kusanywa. Ni kwa kupitia Uislamu pekee ndipo usawa utakapo patikana. Katika toleo lililo andikwa na Jamal Harwood mnamo 7 Machi 1999, alieleza kuwa "Sera kuu ya kiuchumi ya dola ya Khilafah ni kukidhi mahitaji msingi ya jamii yenye afya na yenye kupanuka. Uislamu unalifafanua tatizo kuu la kiuchumi kuwa ni ugavi na wala si uzalishaji kama urasilimali unavyo fanya. Hili lahitaji utafautishaji wa wazi kati ya mali ya dola, ya umma na inayo milikiwa kibinafsi. Angazio kuu la dola ya Khilafah litakuwa namna ya kusambaza nguvu-kazi yake, utajiri na rasilimali kuanzisha "mapinduzi" katika viwanda vizito, utengezaji wa bidhaa na usambazaji." Kutekelezwa kwa ushuru wa sasa juu ya mapato badala ya ushuru juu ya mali, kama ulivyo wajibishwa na Uislamu ni jambo kuu linalo vunja moyo uwekezaji na uimarishaji. Kuna kishajiisho sahihi cha uwekezaji kamilifu kwani mali isiyo tumiwa hutozwa ushuru kupitia Zaka au yaweza kukusanywa kwa ajili ya matumizi muhimu ya dola. Kwa hayo, uchumi wa Kiislamu ni wenye nguvu mno, ulio na sifa ya uwekezaji kamilifu na mzunguko wa mali wa hali ya juu.

**Kassim Agessa**
**Mwanachama wa**
**Hizb ut Tahrir Kenya**

# Hali ya Kisiasa Nchini Kenya: Mgogoro wa Demokrasia




Macho yote ulimwenguni mnamo Jumanne 30 Januari 2018 yalielekezwa nchini Kenya, kitovu cha Afrika Mashariki, huku Muungano wa NASA ukianza safari ya kuonyesha uasi kwa utawala wa Jubilee na kinara wake Raila Odinga kula "kiapo" kilicho waacha wengi kujiuliza maswali juu ya hatua yake ya kisiasa itakayofuata. Bwana Odinga alijiapisha kama "Raisi wa Watu". Akitaja dhulma za uchaguzi, Odinga alisusia uchaguzi wa Oktoba mwaka jana uliopelekea Bwana Uhuru Kenyatta kutangazwa kama Raisi wa Jamhuri ya Kenya ambaye kulingana na matokeo ya Tume ya Uchaguzi ya IEBC alishinda kwa asilimia 98% ya kura zote zilizopigwa.

Ili kufahamu hali hii ya kisiasa na maana yake twahitaji kuangazia matukio yafuatayo:

**Kwanza;** Baada ya uchaguzi wa Oktoba, Uingereza ilikuwa serikali ya kwanza kumpa hongera Raisi Uhuru Kenyatta baada ya ushindi wake kuidhinishwa na Mahakama ya Upeo mnamo Novemba mwaka jana. Waziri wa Kigeni wa Uingereza Boris Johnson alituma risala ya nchi yake katika maongezi ya simu na Waziri wa Kigeni (wa Kenya) Amina Mohammed. Muungano wa Ulaya uliwaomba wanasiasa kutambua kuchaguliwa tena kwa Raisi Kenyatta na kuheshimu katiba na sheria. Amerika ilitoa wito wa kuwepo kwa mazungumzo ya kitaifa ili kumaliza mtafaruku.

**Pili:** Mnamo Ijumaa 16 Januari bunge la Muungano wa Ulaya lilijadili ripoti juu ya uchaguzi wa Kenya iliyo tolewa na mkuu wa waangalizi wa uchaguzi wa muungano huo Mariette Schaake jijini Brussels kuwa uchaguzi wa Agosti ulikumbwa na dosari. Haya yalikinzana na ripoti yake ya awali iliyotolewa mnamo Agosti ambayo ilipongeza kuwepo kwa uwazi katika uchaguzi huo.

**Tatu:** Mnamo 26 Januari Umoja wa Mataifa ulithibitisha kumtuma aliyekuwa Raisi wa Nigeria Olusegun Obasanjo ambaye ni mwanachama wa Jopo Kuu la Upatanishi la Katibu Mkuu wa Umoja huo ili kuleta upatanishi katika sintofahamu ya kisiasa nchini Kenya. Msemaji wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, Stephaney Dujarric, akijibu maswali kutoka kwa chombo cha habari cha City Press jijini Geneva mnamo 19 Januari 2018, alithibitisha kuwa kwa yakini walimtuma Obasanjo nchini Kenya. "Kama mujuavyo, hali ya kisiasa nchini Kenya tumekuwa tukiifuatilia kwa karibu, hususan matayarisho yanayo endelea ya upinzani, muungano wa NASA, ya kuapisha yaliyo pangwa kufanyika mnamo Januari." Licha ya kuthibitisha kwa msemaji huyu, Jubilee na NASA zilikana kuwa na ufahamu kuwa Obasanjo alikuwemo nchini kwa ajili ya upatanishi. Kiongozi wa wengi katika bunge la kitaifa Aden Duale alikana kuwepo kwa mkutano kama huo huku msemaji wa ikulu Manoah Esipisu akikataa kujibu wakati alipoulizwa kuhusu mkutano huo.

*Endelea Uk..9*

**Nne:** Vinara wa NASA walifanya mkutano na waandishi habari katika hoteli ya Intercontinental jijini Nairobi na kudai kuwa Raila na mgombea wake mwenza Kalonzo Musyoka walipata kura 8,041,726 dhidi ya kura za Raisi Kenyatta 7,755,428. Haya yalijiri siku tatu kabla ya kuapishwa.

**Tano:** Mwenyekiti wa Tume ya Muungano wa Afrika Moussa Mahamat alitoa ombi la kuwa mpatanishi baina ya Raisi Kenyatta na Bwana Odinga ili kutatua mtafaruku wa kisiasa unaoendelea kukua. Bwana Mahamat alizisihi pande zote kujiepusha na vitendo vitakavyo yaweka maendeleo ya Kenya hatarini.

**Sita:** Serikali ilivifungia vyombo vya habari na hata kuwatishia baadhi ya wanahabari. Siku chache tu baada ya usanii wa uapishaji, ghasia zilizuka katika mitaa ya Kibera magharibi mwa Nairobi na baadhi ya maeneo ya Nyanza, ambapo wafuasi wa upinzani waliandamana kupinga dhidi ya kukamatwa kwa mbunge wa jiji, Timothy Kajwang pamoja na Miguna Miguna, wakili aliyekuwa ubavuni mwa Odinga wakati wa sherehe hiyo ya kuapishwa ambaye hatimaye alifurushwa nchini na kupelekwa nchini Canada.

Kadhia tatu zaweza kuvuliwa kutokana na maelezo ya juu: -

A- Raila Odinga bado angali anafurahia uungwaji mkono kote nchini na hususan eneo la Nyanza. Uungwaji mkono wake unampa uzito wa kisiasa katika siasa za Kenya. Alishinda katika uteuzi kuongoza muungano wa upnzani shukrani kwa usaidizi wa Amerika uliojitokeza katika taarifa za aliyekuwa balozi mkakamavu wa Amerika Michael Rannaberger aliyetoa wito kwa wapiga kura kumuunga mkono "kijana", akiashiria Raila ambaye ni kijana kwa Kibaki kwa miaka mingi. Mnamo 2007 na 2013, Amerika ilikuwa na uhakika wa ushindi wa Odinga ingawa haukutokea. Mnamo 2017, ilikuwa na shaka juu ya ushindi wake. Kwa kuwa Amerika inapata baadhi ya hisa ya kiuchumi ambayo kwa mujibu wa takwimu za kiuchumi zaonyesha kuwa Amerika imeipiku Uingereza kwa mara ya kwanza kama chimbuko la watalii wa kigeni waliozuru Kenya mnamo mwaka huo kuanzia Oktoba 2016, hivyo kuimarisha msimamo wake kama chimbuko muhimu la mtiririko wa dolari nchini ikiongezewa na mtiririko wake kutoka ng'ambo, na hivyo basi kutomjali Odinga. Hii ndio sababu Amerika ilishutumu kuapishwa kwa Raila Odinga kama raisi wa watu. Katika taarifa ya mnamo Alhamisi 1 Februari, Amerika ilitaja: "Tunapinga vitendo vya kuhujumu katiba na sheria za Kenya. Uhuru Kenyatta alichaguliwa kama raisi wa Jamhuri ya Kenya mnamo Oktoba 26, 2017 katika uchaguzi ulioidhinishwa na Mahakama ya Upeo ya Kenya." Kile anacho fanya Raila kwa sasa ni jaribio tu la kufanya udalali wa kisiasa na kurefusha uhai wake wa kisiasa. Kwa upande mwengine, Jubilee inawaadhibu vijana wa Raila waliorengwa. Hatua ya kuvigandamiza vyombo vya habari ilikusudia kuficha migawanyiko ya hali ya juu ambayo Kenya inaugua.

B- Uingereza imefaulu kudumisha mashiko yake nchini Kenya kwa kuhakikisha kuwa mtu wake Uhuru Kenyatta anadumisha utawala. Ikitambulika kwa ujanja wake wa kisiasa imetumia Mahakama ya Kimataifa ya Jinai kuwaimarisha Uhuruto iliyodhamini ushindi wao katika uchaguzi wa 2013. Katika uchaguzi wa Agosti mwaka jana Uingereza ilikuwa ikitoa onyo kali ya kuzuka kwa ghasia nchini Kenya, hii ilikuwa kwa lengo la kumsukuma Uhuru Kenyatta kutumia nguvu za hali ya juu kuzuia fujo na pia kuudhihirisha upinzani kama unaohusika na ghasia kwa kuwa huenda akapinga uchaguzi huo. Uingereza inaonekana kufanya ujanja kwa kuwa tayari ishapata maslahi yake lakini inajifanya kushinikiza kuwepo kwa mazungumzo. Huku Amerika pia ikionekana kushinikiza kuwepo kwa mazungumzo, hayo huenda yakatokea kwa sharti kuwa sehemu kubwa ya mgao utamuegemea Muingereza. Ni vyema ifahamike kuwa wote Marekani na Muingereza wana mgao sawa katika mtazamo wa kisiasa unaowatosheleza maslahi yao nchini Kenya.

C- Kenya ni nchi iliyo gawanyika pakubwa lakini kidhahiri kuna sera ya ushirikiano kati ya Amerika na Uingereza ili kuchochea vita baina ya raia. Fujo la kisiasa lililoko kwa sasa linatoa taswira ya jinsi nchi hii inavyo kabiliwa na migawanyiko ya kikabila na kimaeneo inayo chochewa na wanasiasa kila msimu wa uchaguzi. Licha ya ulinganizi wa kudumu wa fikra finyo za kizalendo na kikabila, ni wazi kuwa fikra hizi ni dhaifu na hivyo basi kamwe haziwezi kuleta umoja wa kudumu miongoni mwa Wakenya. Licha ya hayo, ukabila, utabaka na umajimbo ni karata za kisiasa za kumakinisha au kukwea uongozi. Lakini, kugunduliwa kwa mafuta nchini huenda ikaongeza "chachu" katika mtafaruku ulioko huku Uingereza na Amerika zikionekana kushindana kwa hali ya juu kupata mafuta ya Kenya kwa ajili ya kampuni zao za kimataifa.

Kwa kutamatisha, vita baina ya NASA na JUBILEE si vyengine isipokuwa ni sehemu ya mbinu pana za vibaraka wa warasilimali katika kushindania fursa za kujitajirisha na kujinufaisha kibinafsi huku mtu wa kawaida akiteseka kama mlala hoi! Zaidi ya hayo, inadhihirisha kufeli kwa Demokrasia kuliko itumbukiza Kenya ndani ya majanga yaliyoko sasa. Hali hii ya kisiasa ni mfano mwengine wa mgogoro ulioundwa na Uingereza na Amerika barani Afrika, bara lililobarikiwa na madini mengi lakini kuangamizwa kutokana na ulafi wa wakoloni kupitia vibaraka wao.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa**
**Hizb ut Tahrir Kenya**

# Usivutiwe na Mapambo ya Dunia Hii ya Mapito



Usihofu kuhusu dunia na vilivyomo ndani yake, kwani bila shaka mauti yataichukua pamoja na sisi. Yeyote ambaye hamu yake kubwa ni kuukusanya ulimwengu, siku moja atajuta na kuipa mgongo. Nafsi haitatosheka na ukusanyaji mali za dunia, mahitaji msingi ndiyo yatakayo tosheleza.

Fanya kazi kwa ajili ya maisha ya milele, ambayo bawabu wake ni Ridhwan, jirani yake ni Ahmad na mjenzi wake ni Rahmani. Sakafu yake imetengezwa kwa dhahabu, mchanga wake kwa miski na nyasi zake kwa zafarani. Mito yake ni ya maziwa na asali safi, na tembo, zinazo tiririka kwa usafi katika mito hiyo, huku ndege wakiruka katika vitagaa vyake, wakimsabihi Allah, waziwazi, wakiimba kwa kumsifu. Ni nani anayetaka kununua sehemu katika bustani la kifahari la Eden, katika kivuli cha Tubaa (mti), ndani ya majumba yake ya kifahari? Ni nani anayetaka kununua sehemu ndani ya Firdaus, kwa mnada wa Rak'a moja kwa kivuli cha usiku unaomfinika? Au kwa kumlisha masikini mwenye njaa mpaka ashibe katika siku ya ukame na vita?

Nafsi imetosheka na dunia ilhali inajua fika kuwa usalama na furaha ndani yake ni kuvipa mgongo vilivyomo ndani yake. Wallahi! Ikiwa nafsi itaridhika na kile ilicho ruzukiwa, itatoshelezeka nacho. Wallahi! Wallahi! Ni usalama, narudia tena mara ya tatu. Lau kungekuwa na jiwe laini ufuoni mwa bahari, ingeliosha eneo lake (kwa kiasi cha maji kinachotaka). Allah ameahidi kumpa mja riziki yake, mpaka aipokee yote. Vile vile, lau kungekuweko na barabara juu ya mbingu ya saba, Allah angetoa njia itakayo ishukisha (kumfanya apate riziki hiyo) kwa urahisi. Hadi upate lile lililo andikwa katika Lawh al-Mahfudh, ikiwa bado hujaipata, bila shaka utaipata.

Pesa zetu tunazo zilimbikiza zitarithiwa. Na ardhi yetu ambayo ikaribu kuangamia itajengwa. Hakuna mahali pa mtu kupumzika baada ya kufa kwake isipokuwa pale ulipo pajenga kabla. Chuma matunda ya kesho mahali pema, pasipo karibiwa na fedheha wala karaha. Ndani yake muna starehe, zenye kudumu milele na milele, zisizo na mwisho wala kufukuzwa kutokana nazo. Hakuna masikio wala macho yaliyowahi kuziona au kuzisikia, wala moyo uliowahi kuvuta taswira yake. Kwa hivyo hongera! Kwa kupata hadhi kwa mwenye kuipata na hongera kwa nafsi zitakazo kuwemo ndani yake.

Na usihadaiwe na mahali hapa (ulimwenguni) na starehe zake kwani karibuni yanayo kuzuzua yatatoweka. Idhibiti nafsi yako usidanganywe na mapambo yake na tahadhari na mitego yake mikuu. Uhadaifu wake haukudumu zaidi ya siku moja kwa yeyote, wala hawakusimama imara dhidi ya usiku wake. Hivyo basi tazama na tafakari jinsi gani wengi wameangamia kwa ghafla na ni watu wangapi ambao wameshambuliwa na mshale wa mauti? Qaroon alijifakhiri kwa mali yake kutokana na ujinga wake na kulevywa nazo; aliwaita watu wake kuitizama. Alikesha usiku kucha, kutafuta mali bila ya mapumziko na hamu yake ya kumiliki. Na mchana, ulikuwa ni janga kwake uliotia moyoni mwake hamu na hivyo basi kuificha.

Kwa hivyo yeyote atakaye ijenga kwa wema (atakaye zitumia pesa zake katika kheri) malipo yake yatakuwa mazuri, na yeyote atakaye ijenga kwa maovu, yataangamia makaazi yake. Majumba haya yaliyoko ardhini yatagurwa na kuwa magofu na majengo yake kuonja mauti. Wako wapi wale wafalme ambao neema ziliwafanya kutakabari mpaka Mwenye kuwaneemesha kuwaonjesha kinywaji cha mauti. Vizazi na vizazi vimezikwa na hivyo hivyo kila mwenye uhai leo pia. Tahamaka, mauti huzika kila mtu ndani yake (ulimwengu). Hivyo basi, mauti yanaukodolea macho ulimwengu na uhadaifu wake huku watu wakiendelea kutojali kujiweka mbali kutokana na vilivyomo ndani yake. Isipokuwa wakati nia zake halisi zitakapo dhihiri. Hakuna maisha yatakayo kubali siku zake bali yatazikataa. Tumeshughulishwa na kazi zetu na kutafuta dunia kwa gharama ya mauti, ambayo hayana budi kutufika.

**Shairi Kutoka kwa Ali ibn Abi Talib (ra)**
**http://www.saaid.net/Doat/hamesbadr/48.htm**


Email: info@uqab.or.ke

# Wanawake Hawana Hadhi Chini ya Nidhamu ya Kijambazi ya Kidemokrasia

**Habari:**

Vyombo vya habari nchini Kenya vimeangazia habari kuhusu madhila wanayo fanyiwa wanawake (kina mama) katika Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta (KNH) waliokwenda kutafuta huduma za uzazi katika taasisi hiyo kwamba wanadhulumiwa, kubakwa na kufanyiwa vitendo vyengine visivyo semeka na wahudumu wa hospitali hiyo.

**Maoni:**

Mfumo batili wa kirasilimali na itikadi yake ya kisekula humtazama mwanamke kama chombo cha ngono. Hivyo basi, thamani na heshima yao hutegemea uwezo wao katika ngono. Kwa mtazamo huo muovu wanawake wanatarajiwa kuyakabili maisha na changamoto nyingi. Kuongeza chumvi kwenye kidonda; majambazi wa kirasilimali wameeneza hadithi batili kuhusu utetezi wa wanawake ili kupigia debe maslahi ya wanawake. Hiyo imepelekea kuibuka kwa wale wanaoitwa watetezi wa wanawake wanaodai kuwa sauti ya wanawake na kulingania kuhusishwa na kutambuliwa kwa wanawake katika sekta ambazo aidha zimetawaliwa na wanaume au kwa lengo tu la kupigana kumbo na wanaume kwa kile kinachoitwa **usawa wa kijinsia.**

Mvutano wa kupigania kutambuliwa kwa wanawake imepelekea mgongano hatari baina ya mwanamume na mwanamke kwa kuwa nidhamu ya kijamii yenyewe, ambayo ilipaswa kudhibiti mahusiano baina ya mwanamume na mwanamke, yenyewe imefeli kwa kuwa imechipuza kutokamana na akili finyo ya mwanadamu. Hivyo basi, imepelekea kuachwa wazi kwa mujtamaa na kutukuzwa kwa uhuru kama inavyo jitokeza katika nidhamu ya kijambazi ya kidemokrasia hususan **uhuru wa kibinafsi.** Uhuru wa kibinafsi umetoa mwanya kwa wanadamu kutenda chochote wapendacho na mahali popote kwa msingi wa hawaa na matamanio yao. Serikali za kisekula zinang'ang'ana kila uchao kudhamini kupatikana kwa uhuru hizi na hususan uhuru wa kibinafsi, ambao ndio uti wa mgongo wa mujtamaa huu huru wa kisekula.

Ghasia na utovu wa usalama kwa wanawake daima zimekuwa kiwango cha juu na zinaendelea kuongezeka kila mujtamaa unapozidi kuachwa wazi. Hii imetupelekea kushuhudia matukio mabaya kwa mfano:

1. Watoaji huduma za afya kutekeleza vitendo vya kinyama kwa wagonjwa wao wa kike au wanaotafuta huduma hizo vikiwemo ubakaji chini ya uangalizi wao kama vile vinavyo ripotiwa katika kashfa ya sasa katika Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta (KNH). Taasisi maarufu ya afya ya serikali inayo tazamiwa na raia kutoa huduma bora, lakini; badala yake imegeuka kuwa sehemu yenye utovu zaidi wa usalama kwa wanawake kwenda kutafuta huduma ndani yake! Kashfa hii mpya, ambayo siyo ya kwanza kutoa sura ovu ya pango lililo jaa wabakaji, miaka iliyopita pia ilikuwemo machoni mwa watu kutokana na ubadhirifu wa mali wa mameneja wake!

2. Vituo na wahudumu wa afya kuwalazimisha wanawake kuzaa kupitia njia ya upasuaji (CS); ili wapokee mamilioni ya pesa kama malipo kutoka kwa Shirika la Kitaifa la Bima ya Afya (NHIF). Hii imepelekea NHIF kutoa tahadhari juu ya kuongezeka kwa ghafla kwa uzazi wa kupitia upasuaji (CS) ambao pia umepelekea taasisi hiyo kulipa malipo makubwa ya kifedha kwa taasisi za afya zaidi ya kiwango chake cha bajeti. Athari za kiafya za wanawake hazitiliwi maanani; badala yake, manufaa ya kifedha/faida ndiyo yanayo chukua kipaumbele.

3. Wizara ya Afya ya Kenya kutekeleza sera ya mwanamke mmoja kwa watoto wawili, iliyo tokana na nadharia batili inayo pigiwa debe na majambazi wa kirasilimali kwa kutumia mfumo wao batitli wa kirasilimali. Kwamba tatizo la kiuchumi lenye kuwakabili wanadamu ni uhaba wa rasilimali na wingi wa watu, ilhali; ukweli ni kuwa rasilimali ziko za kutosha bali zimelimbikizwa kwa majambazi wachache wa kirasilimali wenye ubinafsi na hivyo tatizo kuu ni jinsi ya ugavi wa rasilimali hizo kunufaisha mujtamaa mzima.

Suluhisho la matatizo yanayowakumba wanawake na wanadamu kwa jumla liko katika kuung'oa mfumo batili wa kirasilimali na kuubadilisha kwa mfumo safi wa Kiislamu utokao kwa Muumba wa viumbe Anayejua zuri na baya kwao. Heshima ya wanawake imekita chini ya bendera ya Uislamu wenye kutekelezwa kama mfumo kamili wa maisha kupitia Khilafah yenye kuongozwa na Khalifah mcha Mungu mwenye kutaraji mabustani ya Pepo ya juu ya milele na na wala sio dunia hii yenye kupita na kumalizika ilojaa maovu! Ni Uislamu pekee utakao linda heshima na dori yake msingi kama mama na mke, na kuwadhamini wanawake haki na majukumu sawa kama wanaume isipokuwa yale yaliyo fafanuliwa na dalili za sheria kuwa ya wanaume pekee na wanawake pekee. Hivyo basi, mwanamke ana haki ya kufanya biashara, ukulima na uzalishaji, kushiriki katika mikataba na miamala; kumiliki aina zote za mali; kuwekeza fedha zake mwenyewe (au kupitia wengine); na kupeleka mambo yake yote ya kimaisha mwenyewe.

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya**
**Hizb ut Tahrir Kenya**



# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 10: Kuvumilia Shida na Maudhi kwa Abubakar Swidiq (ra), Umar Ibnul Khatwab (ra) na Uthman Ibnu Affan (ra) Katika Da'wah

Katika halaqa hii tutaendelea na mbinu ya nne na ya mwisho ambayo wameitumia Maquresh dhidi ya da'wah ya Mtume (saw). Na leo tutazungumzia maudhi na adhabu ambazo wamezipata baadhi ya Maswahaba Radhi za Allah ziwaendee.

**Thabat ya Swidiq رضي الله عنه**

Kutoka kwa Aisha (ra) asema: Walipokusanyika Maswahaba wa (saw) na wakawa wanaume 83. Abubakar alimkokoteza Mtume (saw) watoke wazi.

Akasema: "**Ewe Abubakar! Sisi ni wachache**", basi Abubakar hakuacha kumkokoteza Mtume (saw) watoke mpaka Rasul akatoka wazi. Waislamu wakajigawanya katika vipembe vya msikiti kila mmoja akakaa, ikawa Abubakar ndio mzungumzaji wa kwanza aliyelingania kwa Allah.

Mushrikina wakamshambulia Abubakar na Waislamu, wakapigwa kipigo kikali na Abubakar akakabwa koo kwa nguvu sana na mushrik Utbah Ibnu Rabia'h. Akamsongelea akawa anampiga kwa viatu na kumfutia usoni mwake. Akapigwa Abubakar mpaka pua yake isitambulikane usoni mwake; wakaja Banu Taym na nguo wakamtia nyumbani kwake, wakiamini atakufa...!

Kisha wakarudi Bani Taym wakaingia msikitini Wakasema: "Wallah akifa Abubakar tutamuua Utbah Ibnu Rabiah...! Wakamrudia Abubakar, ikawa Abu Quhafa na Banu Taym wanamzungumzisha Abubakar mpaka akawajibu; alizungumza jioni akauliza: "Mtume (saw) yuko vipi? Hakufanywa kitu Mtume wa Allah?!"

**Wa Kwanza Aliye Tangaza Uislamu Wake**

Amesimulia Is'haaq kutoka kwa Ibnu Umar (ra) asema: Alipo silimu Umar (ra) alisema: "Qureyshi gani nitampelekea maneno haya?"Akaambiwa: Jamil Bin Muammir, Akamwendea, asema Abdullah ibn Umar, nami nikawa namfuata athari yake, na kuangalia anachokifanya na ilhali mimi ni kijana ninaye fahamu kila ninachokiona mpaka alipomfikia. Akasema: "Je unajua ewe Jamil kuwa mimi nimesilimu na nikaingia katika dini ya Muhammad (saw)?" Akasema: Wallahi hakumjibu bali aliinuka na kukiburuta kishale cha umar (ra) na Umar akamfuata, nami nikamfuata mpaka aliposimama katika mlango wa msikiti na kupiga kelele kwa sauti ya juu: "Enyi Maquresh (wakiwa wako katika shughuli zao); Tambueni Ibnul Khattab amewacha dini ya mababu zake...!" Asema: anasema Umar akiwa nyuma yake, amesema uongo, mimi nimesilimu, nikashudia LAA ILAAHA ILLA-LLAH MUHAMMAD RASULU-LLAH! wakamvamia huku wanampiga, basi hawakuacha kupigana mpaka jua likawa utosini mwao!

Asema: Umar alichoka, mwisho akakaa wakamsimamia kichwani naye anasema: "Fanyeni mnachokitaka, naapa kwa Allah lau tungekuwa waume 300, tungewaachia mji ama mtuachie...!" Asema: Walipokuwa katika hali hiyo akatokea mzee wa kiquresh (Al-Aas bin Waail As-Sahmiy) Akiwa na vazi zuri, na kanzu nyeupe akawasimamia na akasema: "Mna nini?" Wakasema: "Umar amewacha dini ya wazee wake", akasema, "Nyamaza...! Mtu amejichagulia jambo kwa nafsi yake mwataka nini? Mnadhani Baniy Adiy watawaacha mumuuwe huyu mwenzenu?Mmwacheni huyu mtu...!" Asema: Naapa kwa Allah kana kwamba walifunuliwa pazia.

**Thabat ya Dhin-Nurayn / Uthman**

Amepokea Saa'd kutoka kwa Muhammad Ibnu Ibrahim At-Taymiy asema: Aliposilimu Uthman ibnu Affanرضي الله عنه , Alichukuliwa na ami yake al-Hakam bin Abi al-Aas Ibnu Umayyah, akamfunga kamba. Akasema: "Unaacha Mila za wazazi wako unafuata dini ya mzushi? Wallahi sitakufungua kabisa mpaka uwache haya uliyo nayo kutokana na hii dini...!"Akasema Uthman: "Wallahi sitoiwacha milele ...!" Al-Hakam alipoona misimamo yake katika dini yake Alimuacha...!

**Itaendelea katika UQAB Toleo 15…In Shaa Allah.**

# Matukio ya Kisiasa Ndani ya Kurdistan na Iran

**Swali:**
Mnamo tarehe 06/01/2018, Iran ililituhumu jimbo la Kurdistan kuwepo nyuma ya maandamano ya nchini Iran, na mnamo 07/01/2018 jimbo la Kurdistan lilikanusha tuhma hizi. Kumegunduliwa ripoti za habari wakati wa maandamano makubwa yaliyo fanyika jimbo la Kurdistan, hususan katika mkoa wa Sulaymaniyah mnamo 19/12/2017, zinazo sema kwamba Iran ilicheza dori kubwa katika maandamano hayo. Je, yaweza kusemwa kwamba jimbo la Kurdistan lilikuwa na mkono wake ndani ya maandamano hayo ya Iran mnamo 28/12/2017 kama kesi ya kulipiza kisasi? Kwa maana nyengine:
1- Je, yaliyotokea nchini Iran na katika jimbo hilo ni kama hatua ya kukirudi kitendo? 2- Je, maeneo haya mawili yalichukua hatua za haraka kibinafsi au nguvu kutoka nje iliyasukuma? 3-Ikiwa ni hivyo, nguvu hii ni nani? Je, maandamano haya yanakusudia kubadilisha serikali katika jimbo hilo au Iran? Na Allah akulipe kheri.

**Jibu:**

Matukio mawili haya sio hatua ya kukirudi kitendo, na tuhma za Iran kwa Erbil ni aina mojawapo ya kuchanganyikiwa kisiasa kutokana na natija ya matukio ya ndani. Erbil kwa sasa hivi imeshughulishwa na mgogoro wake, ambao unakaribia kulivuruga eneo lake, na haina uwezo kulingana na dhurufu zake za sasa, kuingia katika barabara za Iran! Kuchanganyikiwa huku kisiasa kulikuwa wazi wakati Iran ilipo zituhumu nguvu kadhaa kwa uchochezi wa maandamano hayo; maafisa wa Iran wamezilaumu nguvu za kigeni. Balozi wa Iran wa Umoja wa Mataifa, Ghulam Ali Khoshro, alisema mnamo Ijumaa: "Kwamba Tehran ina ushahidi mzito kuwa "maandamano" haya yamepokea muongozo wazi wazi kutoka ng'ambo"… (BBC Arabic 07/01/2018). Hivyo basi, tuhma za Iran kwa Erbil zimo ndani ya kuchanganyikiwa huku: (Katibu wa Baraza la Ushauri la Iran, Mohsen Rezai, alisema mnamo 6/1/2018 kuwa maelezo zaidi ya mandhari ya matukio nchini Iran yalipangwa mjini Erbil, jimbo la Kurdistan la Iraq … (Russia Today 07/01/2018). Jimbo hilo limekanusha tuhma hizo kupitia Sven Dzii, msemaji wa jimbo hilo (Chanzo chake kimetangulia kutajwa). Hivyo basi, kadhia sio kukirudi kitendo, lakini kila mmoja ana malengo na masharti yake. Lakini, matukio hayo mawili yalianza kwa ghafla na kisha kuzungukwa na dhamira kutoka nje ili kufikia malengo yanayo husiana na jimbo hilo na Iran. Kuambatana na msururu wa matukio hayo, ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo:

**Kwanza: Matukio Jimboni Humo**

1- Mashirika kadhaa ya habari yaliripoti kuzuka kwa maandamano mnamo 19/12/2017 eneo la Sulaymaniyah, miongoni mwa walimu na wafanyikazi ambao hawakuwa wamelipwa mishahara yao kwa muda wa miezi kadhaa, na kisha maandamano hayo yakajumuisha sehemu kubwa ya wakaazi wa mkoa wa Sulaymaniyah, na kisha kuenea sehemu nyenginezo za mkoa huo zikiwemo sehemu za mkoa wa Erbil. Kujihusisha kwa haraka kwa raia katika maandamano haya ni natija ya watu kutoridhika na hali ya kiuchumi ya jimbo hilo baada ya kushuka kwa kiwango cha rasilimali kuu za mafuta jimboni humo kutokana na Baghdad kuudhibiti mkoa wa Kirkuk pamoja na shinikizo nyenginezo zilizotiwa na Baghdad, hususan kufungiwa kwa ndege za kigeni kutua viwanja vya ndege mikoani Erbil na Sulaymaniyah, iliyoongezea matatizo ya usafiri kuelekea ng'ambo, huku ikiwalazimu wasafiri kusafiri kupitia uwanja wa ndege wa kimataifa wa Baghdad. Kilichotia msumari wa moto kwenye kidonda ni tuhma za ufisadi na ufujaji mali dhidi ya maafisa wa serikali wenye ushawishi mkubwa jimboni humo. Maandamano hayo yalisambaa kama moto nyikani, hususan katika maeneo ambayo ushawishi wa vyama vya Kikurdi dhidi ya Masoud Barzani na Chama chake cha Kidemokrasia cha Kurdistan ni mkubwa. Kuhama kwa familia za Kikurdi kutoka Kirkuk na kwengineko na kuja jimboni humo kumechochea kuzorota kwa hali mbaya za kimaisha huku kukiwa na hofu ya kuzuka kwa harakati pinzani ndani ya jimbo hili. Yote haya yanaashiria kuwa harakati hizi ni za kihamasa.

2- Maandamano haya yaliongozwa kimsingi dhidi ya serikali ya mkoa wa Erbil, inayo dhibitiwa na Chama cha Kidemokrasia cha Kurdistan, chama cha Barzani, aliye mafichoni baada ya kujiuzulu kwake kutokana na uraisi wa eneo hilo nyuma ya mpwa wake Nechirvan Barzani, na hili hufahamika kwa namna nyingi, zikiwemo:
A – Maandamano haya yalizuka kuanzia mkoani Sulaymaniyah, mkoa unaodhibitiwa na harakati na vyama vinavyo mpinga kibaraka wa Uingereza Masoud Barzani. Ngome ya vuguvugu la mabadiliko ni mkoa wa Sulaymaniyah, na tawi lenye nguvu la Talabani ndani ya Chama cha Umoja wa Kizalendo ni mkoa wa Sulaymaniyah vile vile. Vyama hivi vina uwezo wa kuchochea na kuandaa matukio ingawa havina uwezo wa kudhibiti matukio yote.
B – Taarifa ya Nechirvan, inafahamika kana kwamba maandamano hayo yanaongozwa dhidi ya serikali yake: "Raisi wa serikali ya jimbo la Kurdistan, Nechirvan Barzani, ameonya kuwepo kwa "njama kubwa" iliyo anzishwa dhidi ya jimbo hili na ni kubwa mno iliyopita taswira ya mtu yeyote", na akagusia kuwepo kwa "vyama vinavyotaka kuleta fujo katika jimbo hilo na kuyapoteza mwelekeo maandamano hayo na kueneza ghasia". Aliongeza kusema: "Kuna mikono fiche nyuma inayo jaribu kusababisha fujo katika Kurdistan na tutazima jaribio hilo," akikusudia vyama hivi, ambapo hakuvitaja

Endelea Uk..14

majina, “vinavyo unga mkono juhudi hizo za kuzua fujo, lakini halmashauri za kiusalama jimboni humu zitakabiliana vikali na hali hizi…” Alifafanua kuwa: “Tunakabiliwa na tishio hatari na njama kubwa zaidi ya taswira ya mtu yeyote, yaliyotokea katika mkoa wa Sulaymaniyah ni majaribio ya kuhujumu usalama na utulivu,” akitoa wito wa haja ya umoja na ushirikiano kwa wote kuweza kuyadhibiti haya. (Tovuti ya Kurdish Basnews, 21/12/2017)
Kwa maneno haya anajaribu kuvifahamisha vyama vya Kikurdi vinavyo pinga vikali kura ya maamuzi mkoani Sulaymaniyah, na vilivyo na mafungamano na Waamerika na wafuasi wao katika miji mikuu ya Baghdad na Tehran. Kutokana na vyama hivyo vilivyo chochea upinzani na maandamano dhidi ya serikali ya Barzani: vugu vugu la mabadiliko, lililozuka baada ya kugawanyika kutoka kwa Muungano wa Kitaifa msukumo wa pili wa kisiasa katika uchaguzi wa 2009 jimboni Kurdistan. Baada ya upinzani huo, vugu vugu hilo la mabadiliko, lililoongozwa na Gorran na kundi hilo la Kiislamu, lilijiondoa kutoka katika serikali ya Erbil, na kinara wa kundi hilo, Yassin Hassan, alisema katika mahojiano na Al Jazeera, “Baada ya kuwafyatulia risasi waandamanaji, kundi hilo la Kiislamu na vugu vugu la mabadiliko yaliamua kujiondoa kutoka kwa serikali hii kikamilifu, na hivyo tunataka kuvunjiliwa mbali kwa serikali hii mara moja na kuundwa kwa serikali ya uokovu wa kitaifa.” (Al Jazeera Net 21/12/2017)
Shirika la habari la BBC mnamo 26/12/2017 pia liliripotia msimamo wa mmoja wa viongozi wa vugu vugu hilo la mabadiliko, Yusuf Muhammad, na Raisi wa bunge la jimbo la Kurdistan nchini Iraq. Alijiuzulu ili kudhaifisha msimamo wa serikali ya Erbil mbele ya upinzani; Raisi huyo wa bunge la jimbo la Kurdistan nchini Iraq alitangaza kujiuzulu kwake kupinga dhidi ya kile alicho kiita kudhibitiwa mamlaka halali na kikundi au vikundi vya watu fulani pekee. Yusuf Muhammad alikikashifu vikali kikundi hicho cha watu juu ya kudhibiti siasa, uchumi, ardhi, mali na nyanja zote za maisha, pamoja na ubaguzi katika ugavi wake jimboni humo. Alisema kuwa kukataa kwa Amerika kura hiyo ya maamuzi, iliyo wakilishwa katika barua iliyo tumwa na Waziri wa Kigeni wa Amerika Rex Tillerson ni fursa ya dhahabu iliyopotezwa na serikali ya jimbo hilo… (BBC 26/12/2017) Hiki ni kiashiria cha utiifu wa bwana huyu na vugu vugu lake.

3- Hivyo basi, kuanza kwa maandamano kuanzia mkoa wa Sulaymaniyah, yaliyo ongozwa na vyama pinzani kwa Chama cha Kikurdi cha Kidemokrasia cha Barzani, kushiriki kwa viongozi wa wa vyama hivi katika maandamano haya, kukamatwa kwa baadhi ya viongozi hao na majeshi ya usalama, kujiondoa kwa vyama hivi kutoka katika serikali ya Erbil ili kuidhaifisha, kulingania kuvunjiliwa mbali kwake, kujiuzulu kwa kinara wa bunge miezi michache kabla tarehe iliyo pangwa ya uchaguzi, na tishio la Al-Abadi jijini Baghdad la kuingilia kati, yote yanaashiria kuwa mwanzo, ingawa ghafla, una mwelekeo wa pili wa malengo yatokayo nje yanayolizunguka vugu vugu hili la kimaumbile ili kufikia malengo yanayo husiana na jimbo hili. Mwelekeo huu wa pili ni natija ya shinikizo la makundi ya kieneo ya upinzani wa Kikurdi dhidi ya ushawishi wa Barzani, pamoja na shinikizo za Baghdad za kuing’oa serikali ya Barzani mkoa wa Erbil. Ikifuatiwa na yale yaliyosikika kutoka Uturuki, Iran na Baghdad ya haja ya kuwaadhibu waliohusika na tukio la kura ya maamuzi ya kuitenga Kurdistan, na vyama vyote hivi na serikali zote hizi ni tiifu kwa Amerika, ikiongezewa katika hili, kinacho shuhudiwa katika sera ya Trump jimboni humo, pamoja na mwito wa “Amerika Kwanza”, ni kuwa Amerika haija tosheka na sera yake inayo tekelezwa maeneo ambayo vibaraka wa Uingereza wanapatikana, bali ikiwa maslahi yao katika baadhi ya maeneo yatahitaji, itawaadhibu au kuwadhalilisha, kama ilivyotokea katika usanii wa kampeni dhidi ya ufisadi nchini Saudi Arabia, na kama inavyo jitokeza leo kwa viongozi wa chama cha Peoples’ Congress jijini Sanaa baada ya kuuwawa kwa Swaleh. Hivyo basi, Amerika inawasukuma vibaraka wake wa kieneo na wa jimboni humo kutia shinikizo zaidi kwa serikali ya Barzani kuing’oa na kumaliza utawala wa Uingereza juu ya serikali ya Erbil. Ikiwa haitaweza kufanya hili hivi karibuni, itaunda dhurufu kwa ajili ya hilo kupitia shinikizo za kufuatana.
**Hili ndilo aghalabu lililotokea na linalotokea jimbo la Kurdistan**

**Pili: matukio nchini Iran**

1- Maandamano yaliyozuka mnamo 28/12/2017 yalianza kupinga hali ya kiuchumi na hali za kimaisha za watu, ukosefu mkubwa wa ajira, umasikini na kiwango kikubwa cha bei za bidhaa; inaripotiwa kuwa kiwango cha ukosefu wa ajira kiko juu mno. Waziri wa mambo ya ndani wa Iran, Abdul Ridha Rahmani Fadhli, alifichua katika mkutano wa waandishi habari mnamo 1/10/2017 kuwa “kiwango cha ukosefu wa ajira kwa sasa kinazidi asilimia 12% huku asilimia hii katika baadhi ya miji ya Iran ikifikia 60%, ikiwemo Ahwaz (eneo la Waarabu) na Kermanshah (eneo la Wakurdi) na Baluchistan. Kiwango hiki cha ukosefu wa ajira miongoni mwa watu wanaomiliki shahada ya sayansi na waliohitimu chuo kikuu kiko juu mno… “ (2/10/2017). Ripoti zinaonyesha kuwa asilimia 21% ya waliohitimu chuoni hawana ajira, na kwamba milioni 15 ya Wairani wanaishi chini ya msitari wa umasikini hii ikimaanisha kuwa natija ya kutekelezwa kwa nidhamu ya kirasilimali athari yake mbaya inajitokeza kwa raia jumla nchini humo kama ilivyo hali katika nchi zote zinazo tekeleza nidhamu hii ya kimagharibi, na kwa kuwa nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali inatekelezwa nchini Iran, ugavi wa rasilimali huko ni mbaya, kuna ulimbikizaji wa mali katika mikono ya matajiri wachache na kuwanyima wengi kutokana na kujinufaisha kwayo. Zaidi ya hayo, huko kuna kufeli katika kukabiliana na kadhia ya umasikini, mabenki huko yanaendeshwa kwa riba, na huko kuna utekelezwaji wa nidhamu ya

*Endelea Uk..15*

kidhulma ya ushuru katika rasilimali iliyo fungamanishwa na sera na mapendekezo ya Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF).
Na kabla ya matukio ya hivi karibuni, ujumbe kutoka Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) ulizuru Tehran mnamo 18/12/2017; daima hufanya mashauriano ya kila mwaka pamoja na serikali ya Iran. Kinara wa ujumbe huo, Catriona Purfield, aliwahutubia maafisa wa Iran: "Kutokana na hali hii isiyo tabirika na kuongezeka kwa hofu katika nidhamu ya kifedha ya Iran, serikali yapasa kuongeza kasi mageuzi katika mabenki na kuongeza mtaji wa mabenki na taasisi za utoaji mikopo. Aliongeza kusema kuwa: "Tathmini ya ubora wa rasilimali inapaswa kuanza kufanywa mara moja, mikopo ya wahusika inapaswa kutathminiwa, na mipango kuanzishwa kuzigeuza rasilimali za benki na kuwa pesa taslimu ili kutatua tatizo la mikopo iliyo telekezwa ulipaji wake… gharama za ugeuzaji huu wa rasilimali za benki zaweza kumudiwa kupitia utoaji bondi za mikopo za serikali," aliongeza kusema (Ukurasa rasmi wa Al-Alam ya Iran 19/12/2017). Na utekelezwaji wa matakwa hayo ya serikali ulisababisha ongezeko la bei, ukosefu wa ajira na umasikini uliyo pelekea watu kuishi katika hali mbaya na maandamano dhidi ya serikali hii, na kupelekea watu kudhihirisha mateso yao kwa njia zote.

2- Maandamano haya yalianzia jijini Mashhad lililo Mashariki mwa Iran, mwito ukiwa "Tunapinga ongezeko la bei," lakini baadaye kuenea hadi miji 80. Maelfu ya vijana na wafanyi kazi walishiriki na walighadhabishwa na maafisa wafisadi, ukosefu wa ajira na kupanuka kwa mwanya baina ya matajiri na masikini. "Maandamano haya yalitokana na mambo matatu: kwanza, ni sera ngumu za IMF katika kufanya marekebisho ya kiuchumi, na pili, udhaifu wa serikali na maafisa wake katika kutatua matatizo ya kiuchumi, na mwisho; kukwepa uwazi na kuhisabiwa katika maamuzi yanayofanywa na serikali," Ahmad Tavakkoli, mwenyekiti wa shirika la uwazi na haki nchini Iran, alisema katika mahojiano na shirika la habari la Fars mnamo 30/12/2017 "Yote haya yanapaswa kuongezewa katika matumizi ya nje ya Iran kwa wanamgambo na wafuasi wao nchini Lebanon, Syria na Yemen.
Hii inalifanya tatizo la kiuchumi kuwa mzigo mkubwa kwa Wairani, mpaka kuwapelekea kuandamana na hata zaidi ya hili; kuituhumu serikali kwa usaliti wa maisha ya raia wake. "Wairani wengi wanaamini kuwa hakuna haja ya serikali yao kulisaidia kundi la Hamas eneo la Gaza, Hezbollah nchini Lebanon, serikali ya Assad nchini Syria, Mahouthi nchini Yemen, huu ni usaliti" (Arabic 21: 01/01/2018). Yote haya yanaonyesha kuwa kuanza kwa maandamano haya ilikuwa ghafla yakihusiana na mambo ya uchumi. Lakini serikali ilikabiliana nayo kwa kutumia nguvu na kupelekea vifo na majeruhi. Baadhi ya ripoti zinaonyesha kuwa idadi ya waliotiwa nguvuni tangu kuanza kwa maandamano hayo mnamo 28/12/2017 imeongezeka na kufikia zaidi ya 1,700. (BBC Arabic 07/01/2018).

3- Inajulikana kuwa maandamano yoyote ya kiuchumi ikiwa yatacheleweshwa kutatuliwa kwake, kwa utatuzi sahihi, hususan ikiwa yatakabiliwa kwa kutumia nguvu, yatafuatiwa na maandamano ya kisiasa, na hayo ndiyo yaliyotokea. Miito ya kisiasa iliongezwa juu ya miito ya kiuchumi dhidi ya serikali na wale wanaoidumisha, na kukashifu uingiliaji kati wa serikali katika vita vya eneo hilo na kutumia mabilioni ya dola juu yake. Maandamano haya yalianza kutawaliwa na miondoko ya kisiasa inayopinga serikali na kushambulia nembo za serikali hii na viongozi wake. Kisha matukio haya yakatumiwa na Ulaya na Amerika; vyombo vya habari vya Ulaya vilionekana kuyashabikia maandamano haya, hususan Uingereza kama shirika la habari la BBC na runinga yake. Kwa upande wake, Raisi wa Ufaransa Macron alisema katika kujibu swali la gazeti la Al-Hayat kuhusu matukio nchini Iran, lililo chapishwa na gazeti hilo mnamo 4/1/2018: "Maandamano hayo yanamulika uwazi katika mujtamaa wa raia wa Iran. Hili lilinifanya kuwasiliana na Raisi Rouhani ili kumkumbusha haja ya kuepukana na ghasia na kuruhusu uhuru wa kujieleza kwa raia. Tutasubiri na kuona ule uwazi unaohitajika kwa Iran kwa jinsi itakavyo kabiliana na waandamanaji hao ili tuweze kuhukumu baadhi ya mambo huku tukifanya maandalizi ya ziara iliyo pangwa ya Waziri wa Kigeni wa Ufaransa, Le Drian nchini Iran na kisha ziara yangu nchini humo." Na akatoa wito wa kuendelezwa kwa mazungumzo ya kudumu pamoja na Tehran. Lakini uingiliaji kati wa Ulaya kupatiliza matukio haya hauna thamani kwa kuwa sio thabiti.

4- Uingiliaji kati ulio na thamani ni wa Amerika. Raisi wa Amerika Trump alituma ujumbe katika ukurasa wake wa mtandao wa Twitter na kusema mnamo 1/1/2018 "Raia wa Iran hatimaye wanapinga dhidi ya ukatili wa serikali fisadi ya Iran. Pesa zote ambazo Raisi Obama aliwapa kwa ubwege zilielekezwa katika ugaidi na "mifukoni" mwao. Raia wana uhaba wa chakula, mfumko wa bei na ukosefu wa haki za kibinadamu, Amerika inatazama." Waziri wa Habari katika ikulu ya White House alisema: "Idara ya Trump inajali mno. Maelfu ya waandamanaji hawa wametiwa gerezani na serikali," akaongeza: "Kamwe hatutanyamaza kimya huku udikteta wa Iran ukigandamiza haki msingi za raia wake na tutawahisabu viongozi wa Iran kwa ukiukaji wowote." (Gazeti la kielektroniki la Iraq 10/1/2018). Wengi wa maafisa wa Amerika, wakiongozwa na Raisi Donald Trump, wamewaunga mkono waandamanaji wa Iran dhidi ya serikali kuanzia siku ya kwanza. Mwakilishi wa kudumu wa Amerika katika Umoja wa Mataifa, Nikki Haley, aliliambia Baraza la Usalama la Umoja huo mnamo Ijumaa kuwa Amerika inawaunga mkono waandamanaji wa Iran, alisema, "Watu wa Iran wanalilia uhuru wao, ufanisi kwa familia zao na hadhi kwa taifa lao,". Wito wa Washington kwa Baraza la Usalama ni dalili wazi kuwa Amerika ndiyo inayo

*Endelea Uk..16*

endesha mawimbi ya maandamano, na kasi ya wito huo iliwashangaza wanachama wa Baraza hilo la Usalama. “Wanachama wa Baraza hili la Usalama walishangazwa na wito wa Haley wa kuitisha mkutano wa haraka wa Baraza la Usalama kujadili maandamano nchini Iran, lililazimika kutia shinikizo kwa upinzani nchini Urusi kuhudhuria mkutano huu,” Mwandishi wa BBC Barbara Pelt. Mjumbe huyo wa Amerika katika Baraza la Usalama alisema kuwa Washington inasimama “pasi na kuyumba pamoja na wale walioko nchini Iran wanaotafuta uhuru wao na ufanisi kwa familia zao na hadhi kwa taifa lao” (BBC Arabic 06/01/2018)

5- Hili linaibua swali: Je, usaidizi wa Amerika kwa maandamano haya nchini Iran unamaanisha kwamba wanafanya katika kuipindua serikali ya Iran? Au ina lengo jengine inalotafuta kupitia kudandia mawimbi ya maandamano nchini Iran? Kujibu hili, tunasema yafuatayo:
Ama kusema kuwa usaidizi wa Amerika kwa hatua hizo ni kwa lengo la kubadilisha serikali sio sahihi kwa sababu wamesema hivyo wenyewe; Naibu Waziri wa Kigeni kwa Iraq na Iran, Andrew Beck, alisema katika gazeti la Al-Hayat lililo chapishwa mnamo 4/1/2018: “Tunazungumzia tu kuhusu kulindwa kwa waandamanaji na mwishowe tunataka kuona mabadiliko katika miondoko ya serikali hii kwa njia zaidi ya moja, lakini haswa kwa waandamanaji” na kusisitiza kuwa “**idara hiyo inataka mabadiliko katika miondoko ya serikali hii na wala haitaki kuibadilisha serikali hio nchini Iran…**” [imetafsiriwa kutoka kiarabu]. Amerika na dori yake katika serikali hio inajulikana; tulitaja hili nyuma katika “Jibu la Swali” mnamo 21/08/2013: (Dori ya Amerika katika mapinduzi ya Iran lilikuwa wazi kuanzia mwanzo… na matendo yote ya kisiasa ya eneo hili yanayo tekelezwa na Iran yote yanaafikiana na miradi ya Amerika …), na pia tulisema katika jibu jengine “Jibu la Swali” mnamo 23/02/2017 (Hivyo basi, dori ya Iran eneo hili ni sera ya Amerika iliyofanyiwa utafiti kwa umakinifu, na kwamba dori hii hupanuka na kunyauka kulingana na matakwa ya sera ya Amerika na kulingana na dhurufu), na kwa hivyo, kutangazwa kwa usaidizi wa Amerika kwa maandamano haya sio kwa lengo la kubadilisha nidhamu ya utawala iliyoko kwa sasa.

6- Hivyo basi ni kwa nini Amerika imelidandia na kulitumia wimbi hili? Hili ni muhimu kwa sababu mbili:

Kwanza, ni kuhamisha purukushani kutoka kwa kadhia ya Palestina na taarifa ya Trump kuhusu Al-Quds “Jerusalem” na kulishughulisha eneo hili kwa kadhia ya Iran. Hilo, ni ili igeuke kuwa adui nambari moja katika eneo hilo, na kisha watu wote kuiangazia Iran na si kwengineko, na kufifisha kuangaziwa kwa umbile la Kiyahudi, mvamizi wa Palestina.

Pili, ni kutafuta uhalalishaji wa kubakia hai kwa vibaraka wa Amerika eneo hili chini ya kisingizio cha kusimama dhidi ya Iran na kuilinda Amerika kutokana na hatari ya Iran. Taarifa ya Trump kuhusu Al-Quds (Jerusalem) na kuwa huu ndio mji mkuu wa umbile la Kiyahudi (ambao ni uadui mkubwa zaidi kwa Waumini) kama tulivyo sema katika toleo letu la 7/12/2017 ni kofi migongoni mwa vibaraka wa Amerika “Al-Quds (Jerusalem) imo ndani ya nyoyo na akili za Waislamu, na kunyamaza kimya kwa vibaraka hao juu ya taarifa ya Trump na kuendelea kwao kuwa vibaraka na kuiridhisha Amerika ni kashfa kubwa kwao … taarifa ya Trump dhidi ya Iran ilikuwa ni kamba waliyoning’inia kwayo kuhalalisha kuendelea kwao kuwa vibaraka wa Amerika licha ya taarifa ya Trump kuhusu Jerusalem … kwa kusema kuwa Trump anasimama usoni mwa Iran, adui mkuu, ni udhuru mbaya kushinda uhalifu.

﴿قَاتَلَهُمُ اللَّهُ أَنَّى يُؤْفَكُونَ﴾

“Allah awaangamizilie mbali! Vipi wanapotoka na haki?” [ TMQ 63: 4]

7- **Huu pengine ndio ufafanuzi sahihi wa yale yaliyokuwa yakiendelea nchini Iran kuhusiana na maandamano yake na taarifa za kutoka ughaibuni, hususan za Amerika.**

Kwa kutamatisha, kuhadaiwa na nchi za kikoloni za kikafiri kwa mustakbali wa biladi za Waislamu imewezekana pekee kwa sababu ya watawala waovu (Ruwaibidha) wanaozitawala na kwamba wao ni watiifu kwa maadui wa Uislamu na Waislamu, na kuwafuata. Mtume wa Allah (saw) amelionya hili katika yale anayosimulia Ahmad katika Musnad yake kutoka kwa Abu Hurayrah kwamba amesema: Mtume wa Allah (saw) amesema:

إِنَّهَا سَتَأْتِي عَلَى النَّاسِ سِنُونَ خَدَّاعَةٌ يُصَدَّقُ فِيهَا الْكَاذِبُ وَيُكَذَّبُ فِيهَا الصَّادِقُ وَيُؤْتَمَنُ فِيهَا الْخَائِنُ وَيُخَوَّنُ فِيهَا الْأَمِينُ وَيَنْطِقُ فِيهَا الرُّوَيْبِضَةُ قِيلَ وَمَا الرُّوَيْبِضَةُ قَالَ السَّفِيهُ يَتَكَلَّمُ فِي أَمْرِ الْعَامَّةِ

“Kwa hakika watu watajiliwa na miaka ya uhadaifu; mrongo atasadikishwa na mkweli atakadhibishwa; khaini ataaminiwa na mwaminifu atafanywa kuwa khaini; na Ruwaibidha ndio watakaotamka (maamuzi). Ikaulizwa: Ruwaibidha ni kina nani? Akasema: Watu masafihi wanaozungumzia juu ya mambo jumla ya Umma.” Imesimuliwa na Al-Hakim katika Al-Mustadrak na kuiorodhesha kama Hadith Sahih. Matatizo ya Umma huu ni watawala wake, lakini ni Umma bora ulioletwa kwa wanadamu; hautabakia kimya kwa muda mrefu juu ya utawala dhalimu wa Ruwaibidha hawa. Mtume wa Allah (saw) ametupa bishara njema ya kurudi kwa Khilafah Rashida baada ya utawala huu dhalimu kama ilivyotajwa katika Musnad ya Imam Ahmad na At-Tayalisi kutoka kwa Hudhayfah ibn Al-Yaman:

«... ثُمَّ تَكُونُ مُلْكًا جَبْرِيَّةً، فَتَكُونُ مَا شَاءَ اللَّهُ أَنْ تَكُونَ، ثُمَّ يَرْفَعُهَا إِذَا شَاءَ أَنْ يَرْفَعَهَا، ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَى مِنْهَاجِ نُبُوَّةٍ»

“Kisha kutakuwepo na utawala wa utenzaji nguvu, utakuwepo kwa muda apendao Allah uwepo, kisha atauondoa atakapo penda kuuondoa, kisha itakuwepo Khilafah katika njia Utume” kisha akanyamaza.

وَيَقُولُونَ مَتَى هُوَ قُلْ عَسَى أَنْ يَكُونَ قَرِيبًا

“…na wanasema, “Lini litakuwa hilo?” Sema, “Asaa likawa hivi karibuni” [TMQ 17: 51]

**24 Rabii’ Al-Akhir 1439 H**
**11/01/2018 M**